**EPISODE 8 "MAKING RESPONSIBLE DOWNLOADS"**

| | |
|---|---|
| **SCRIPT WRITER** | **Njoki Muhoho** |
| **EDITOR** | **Jan-Philipp Scholz** |
| **KISUAHELI:** | **Eric Ponda** |

**CHARACTERS**

| | |
|---|---|
| **ANNOUNCER** | Male Adult |
| **ZAPCOM** | A 23-year-old computer geek, by village standards. |
| **GEORGE** | 20 years old. Waits tables at his Uncle Kilu's restaurant. |
| **UNCLE KILU** | 55 years old. George's uncle, owner of KULA TU FOODS. |
| **MANAGER** | 45 years old, the local government telecommunications company manager. Everyone calls him The Manager. |

**INTRO**

1. **MUSIC: THEME MUSIC**

*2.* **ANNOUNCER** HUJAMBO MSIKILIZAJI WA DEUTSCHE WELLE MAHALI POPOTE ULIPO NA KARIBU KWA MAKALA NYINGINE YA MFULULIZO WA MCHEZO HUU WA REDIO 'LEARNING BY

EAR' 'NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO' TUKIWA BADO TUNAZUNGUMZIA MASUALA LA TEKNOLOJIA MPYA YA HABARI NA MAWASILIANO KATIKA KIPINDI HIKI CHA 8 KWA JINA "HATUA ZA KUCHUKUA KABLA YA KUINGIA MTANDAONI" YAANI **'*MAKING DOWNLOAD DECISIONS'.***

KATIKA KIPINDI KILICHOTANGULIA, KOMPUTA ZINAVAMIWA NA VIRUSI. KIMSINGI KUNDI LA VIJANA HAWA WAFAHAMU KWAMBA NI MUHIMU WAKATI WOTE KUWA NA KINGA AINA YA ***FIRE WALL*** NA NYINGINEZO DHIDI YA VIRUSI KATIKA KOMPUTA ZAO.WANAKUMBWA NA WAKATI MGUMU KUSAFISHA KOMPUTA HIZO KABLA KUENDELEA NA HUDUMA ZAO.PIA BADO KUNA SUALA LA WIZI WA MUZIKI UNAOREKODIWA KUTOKA KWA MTANDAO NA KUUZWA. SUALA HILO LIMEZUA HOJA ZA KISHERIA NA KADHALIKA KIMAADILI.INGAWA HOJA HIZO AWALI ZIMEPINGWA VIKALI NA VIJANA HAO, KUNDI HILO SASA LIMEANZA KUTAFAKARI SUALA HILO.

PIA ZAPCOM NA WENZAKE BADO WANAKUMBWA NA CHANGAMOTO, JE NI CHANGAMOTO GANI? ENDELEA KUWA NASI HADI MWISHO WA KIPINDI UPATE KUFAHAMU NI CHANGAMOTO ZINAZOWAANDAMA.

**3. A-SFX: SOUNDS OF AN AFRICAN NIGHT. HEAVY BREATHING. DOOR HINGES SCREECH.**

**SCENE 1: KULA TU FOODS AT NIGHT**

**4. UNCLE KILU** **(MUTTERING TO HIMSELF)**…Ama kwa hakika nimezeeka …….! Ilikuwaje nikaiacha hapa?…. uhhhh … na sasa nalazimika kurudi tena hapa mgahawani usiku huu wa giza…! ahaaaah……. kweli nimeanza kuzeeka……..!

**5. B-SFX: DOOR OPENS. SUSPICIOUS MURMURING IN THE BACKGROUND.**

**6. UNCLE KILU** (**MUTTERING TO HIMSELF**) Wale wote wanafanya nini pale pembeni…..? Kwa nini wameizingira komputa moja… saa hizi..? Na usiku wa kiza namna hii…..? (**HE CREEPS FORWARD**)

7. **C-SFX: A POWER SWITCH GOES ON**

8. **UNCLE KILU** Mnafanya nini hapo usiku huu?

9. **D-SFX: LOUD GASPS. SHOCK. QUICK FEET RUNNING AWAY.**

10. **UNCLE KILU** (**SHOCKED)** Nini kinachowashangaza? Mnafanya nini hapo? (**MOVES QUICKLY TOWARDS THEM)**

11. **GEORGE** **(SOUNDING GUILTY AS SIN)** Hakuna kitu,…. Hatufanyi kitu mjomba.

12. **CHORUS** Hakuna kitu ….! hakuna kitu….! kweli hatufanyi kitu…..!

13. **UNCLE KILU** (**MORE SUSPICIOUS THAN EVER**) George, unaficha nini?

14. **GEORGE** Sifichi kitu …. Si kitu … Ni Komputa tu…! Si unajua komputa… ni hizi komputa zetu…!

15. **UNCLE KILU** (**AUTHORITATIVELY SHOVES HIM OFF**) Hebu nionyeshe. nataka kuona hicho mnachodai siiii kitu!. (**SILENCE… DEEP BREATH)**

16. **CHORUS** (**GASPS, THEN SILENCE**)

**17. UNCLE KILU** (**HORRIFIED**) Hata hamuoni aibu…? mnafanya nini hapo? Kutazama picha za uchi wa watu zilizojaa uchafu… ooh Mungu, utusamehe dhambi zetu…! hebu …nione uchafu huo kwenye skrini … ! Toeni haraka… sitaki kuuona uchafu huu tena machoni mwangu.. uondoeni kabla… kabla uchi wa picha hizi …kunipofusha!… (**REMORSELY**) …Mungu nisamehe kwa kuona uchi wa vijana wa rika la watoto wangu…! Mnafanya nini sasa?

**18. VOICE** (**GIGGLE**)

**19. UNCLE KILU** (**LIVID MAD**) Si jambo la kufurahisha? George, umeniudhi sana!. Hivi sivyo nilivyokulea? Kutazama uchafu huu… !watu wakiwa uchi….! Kwa mila na desturi yetu, ni miko kutazama picha hizi za kuchukiza mno. Mmekuwa mkifanya hivi kwa muda gani….? Tokeni nje haraka ….nyote.. nyote tokeni nje…. nje…. nje nyote….!

**20. GEORGE** Mjomba, lakini bado naendelea na zamu yangu ya usiku … bado tunaaaa…….

**21. E-SFX: POWER CABLES AND SOCKETS BEING ROUGHLY UNPLUGGED. CHAIR CRASHES.**

**22. UNCLE KILU** Toka nje..! zamu yako umeishia hapa !.sitaki tena kuona upuzi huu katika mkahawa wangu!. Tokeni nje nyote….. haraka…. Na kisha mutoe hizi komputa zenu hapa….. zitoeni nje…. Nje… nyote nje haraka….!

**23. GEORGE** Lakini mjomba.

**24. UNCLE KILU** Usiniite mjomba tena. Sitaki tena kushirikishwa na… na upuuzi huu katika mkahawa wangu….! (**DISGUST**). Kuanzia leo naufunga!

**25. ANNOUNCER** Labda pengine mjomba Kilu ni mtu aliyepitwa na wakati, lakini kuna mambo ambayo hawezi kukabiliana nayo. Picha za watu walio uchi zimemuudhi sana na kinyume kabisa na imani na tamaduni yake. Ameghadhabishwa mno na mchezo unaoendelea katika mkahawa wake. Na zaidi ana wasiwasi kwamba teknolojia ya sumu itachafua zaidi akili za vijana hawa.

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**26. SCENE TWO: PAVEMENT OUTSIDE KULA TU FOODS**

**27. F-SFX: OCCASIONAL CAR PASSES BY. PATHWAY FOOTSTEPS. SOUNDS OF SOMEONE SHIVERING FROM COLD.**

**28. ZAPCOM** (**SHOCKED**) George, nini kinachoendelea hapa? Mnafanya nini? Kwani mumehamisha huduma kutoka ndani ya mkahawa wa Kula Tu Foods hadi langoni! Hizi komputa zinafanya nini hapa nje …. ? Kwani kumetokea … aaa … moto…? Kwa nini hamkuniita…?

**29. GEORGE** (**VERY MISERABLE**). Ndio … kisha moto mkubwa….!

**30. ZAPCOM** Kwa nini hamkuniita. Nini kimechomeka?

**31. GEORGE** (**MISERABLE**) Kwanza vinena vyetu halafu kichwa cha mjomba Kilu!

**32. ZAPCOM** (**FRUSTRATED**) George, kwani unaanza wazimu? Unazungumzia kuhusu nini?

**33. G-SFX: DOOR OPENS.**

**34. UNCLE KILU** Wewe!… wewe … Njoo hapa ndani upesi!

**35. ZAPCOM** (**WHISPERING TO GEORGE**) George, umefanya nini ?

**36. GEORGE** Si mimi !

**37. ZAPCOM** (**FRUSTRATED**) Ni nani!, mumeanza mbinu za kuniibia!. Umefanya nini?

**38. GEORGE** Alikuwa akitazama…!

**39. UNCLE KILU** Kama hungefika haraka, ungepoteza kila kitu. Hengekuwa na cha kutegemea siku za usoni.

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**40. ANNOUNCER** Mjomba Kilu ni mtu mwenye kulinda hadhi na heshima, lakini zaidi biashara yake, je atafaulu? Sasa anahitaji mtaalam kumshauri kuhusu suala hili. Tayari amewaita wateja anaowategemea, na pia Meneja wa mawasiliano. Ingawa sasa ametimu umri wa miaka 40 na zaidi, mtaalam wa masuala ya teknolojia mpya ya mawasiliano, si mtu wa maneno mengi .

**41. UNCLE KILU** Bwana meneja, hebu waeleze hawa vijana, kwani naamini pia wewe unatumia huduma hizi za Intaneti ofisini mwako, lakini sidhani unafanya mambo haya haya. …?

**42. MANAGER** Usiwakasirikie mzee. Bado ni vijana, na hukosea.

| | | |
|---|---|---|
| **43.** | **UNCLE KILU** | Lakini sisi ni washirika wa kibiashara, na mambo haya yataathiri sana biashara yangu…… mbali na hayo ni watoto wangu pia…. Kwani hivi ndivyo watoto wanavyolelewa siku hizi? |
| **44.** | **Manager** | Pia mimi nina watoto wa kike na wa kiume. Enzi ya sasa ni nyingine, siku hizi maisha yamebadilika sana mzee! Watoto wa siku hizi wanasoma na kuelewa mambo mengi haraka sana. Kwa hivyo usiwakasirikie… hebu subiri kidogo…labda…kimsingi, jukumu letu mimi na wewe ni kuwapa ushauri na muongozo bora. |
| **45.** | **ZAPCOM** | Samahani sana Mzee …tafadhali usitufukuze hapa! |
| **46.** | **UNCLE KILU** | Mimi nimemfukuza hapa… nimemwambia muende. hamkusikia? |
| **47.** | **MANAGER** | (**PLEADING**) Tafadhali Mzee hawa vijana wamefanya juhudi kubwa sana. Kwa hakika nimefurahishwa na kazi yao. Wana uwezo wa kufanya mambo makubwa zaidi. Mzee kila jambo geni lina changamoto zake. Vijana wa enzi ya sasa wanakumbwa na changamoto nyingi kuliko wakati wetu. |

**48. UNCLE KILU** Una maana gani kusema wanakumbwa na changamoto? Unakumbuka enzi zetu tulilazimika kutembea mwendo mrefu hadi mtoni kuchota maji…..heehh…? Siku hizi kuna changamoto gani? (**EMPHATIC**) Kufungua mfereji tu na maji yanatoka. Enzi zetu tuliandika barua kwa mkono na kurudia kila mara unapokosea. Siku hizi ni kupiga chapa tu. Sisi tulikuwa tukitembea maili nyingi sana kupeleka ujumbe…! lakini siku hizi ni kubonyeza tu komputa na ujumbe huo unawafikia zaidi ya watu elfu moja……. Huo si uvivu ni nini? Hawa vijana wameharibika!

**49. MANAGER** Lakini ni watoto wetu! Wanalelewa katika mazingira tofauti sana ya yale tuliyokulia. Jukumu letu sasa ni kuwafunza na kuwapa muongozo, sio kuwapuuza. Hata ukimuona ameketi kando kando ya barabara kwenye baridi kali, bado George ni mtoto wako!

**50. ZAPCOM** (**EXCITED**) Mwambie Bw meneja ….!mwambie!

**51. MANAGER** (**IMPATIENT**) Funga mdomo wako wewe kijana. Hamuwezi kutazama picha zisizofaa eti kwa sababu zinapatikana bure mtandaoni!

**52. ZAPCOM** **(INTERRUPTS)** Lakini si makosa yetu….!. Zinapatikana kila mahali….. kwa kila anayetaka kuzitazama picha hizo…!

**53. MANAGER** **(VERY STERN)** Sasa kwa kuwa zinapatikana kwa urahisi, sio sababu ya nyinyi kupoteza utu wenu?

**54. UNCLE KILU** **(CONTROLLED CALMNESS)** Zapu…Nina wasiwasi sana. Jukumu lako kubwa ni kuwapa muongozo bora hawa wenzio. Wewe ndiye kiongozi wao!

**55. ZAPCOM** Kwa nini? Sina haja ya kupewa majukumu mimi!

**56. UNCLE KILU** Tayari yamemwagika…!.Tufanyeje kuhusu suala hili sasa …! Bado siamini macho yangu kwamba uchafu huu unafanyika hapa katika mkahawa wangu?

**57. ZAPCOM** **(RESIGNED)** Sawa, nitazungumza nao. Sasa mzee naweza kurudisha komputa zangu?

**58. UNCLE KILU** **(FIRM)** Hapana si haraka hivyo! Utazirudisha kwa sharti moja tu…! hakuna tena…uchafu….. Uchafu huo…. …! Na pia umilikaji wangu wa hisa katika biashara hii utaongezeka kwa asilimia kumi.

**59. ZAPCOM** **(SCREAMING)** Haiwezakani!

**60. UNCLE KILU** **(IGNORING THE OUTBURST)** …Mbali na hayo pia mtagharamia bili ya stima …..!

**61. ZAPCOM** **(PLEADING)** Bw Meneja , hebu zungumza naye, tafadhali.

**62. MANAGER** Mimi , ha ha…Simo katika suala hilo. Kila mmoja abebe mzigo wake Zapcom.

**63. H-SFX: FOOTSTEPS LEAVING.**

**64. UNCLE KILU** Na saa nzima ya kuambua viazi kwa angalau wanachama watatu wa timu yenu..kila siku…kwa wiki tatu..

**65. ZAPCOM** Haiwezekani…!

**66. UNCLE KILU** (**MOCKING**) Lakini kwa vile mumenifunza mambo mengi sana ….nitapunguza muda huo kutoka wiki 3 hadi moja… kuambua viazi tu!

**67. MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**68. SCENE THREE: KULA TU FOODS; INTERNET CAFE**

**69. I-SFX: MULTIPLE RAPID TYPING AND MURMURING**

**70. GEORGE** (**LOUD WHISPER**) Sasa biashara imeanza kuimarika tena.

**71. ZAPCOM** (**TROUBLED**) Ndio… lakini tutajuaje kama bado wanaendelea kutazama hizo picha chafu.

**72. GEORGE** Tutawaonya wakomeshe tabia hiyo.

**73. ZAPCOM** Vipi…Sitaambua viazi tena ! (**PAUSE**). Tunaweza kuwashauri kufungua….

**74. GEORGE** **(PANIC IN VOICE, INTERRUPTING**) Eti nini? wewe unawazimu ?

**75. ZAPCOM** **(INTERRUPTS)** … Kutazama tovuti zenye habari ya kuelimisha …

**76. GEORGE** Endelea nakusikiliza….!

**77. J-SFX: SQUEEK OF CHAIR AS ZAPCOM STANDS ON ONE**

**78. ZAPCOM** (**VERY FORMAL**) Habari zenu…? Samahani tulifunga kwa siku chache tu… lakini ni kwa sababu, baadhi yetu walifungua tovuti ambazo ni chafu.

**79. (GIGGLING AND MUMURING)**

**80. ZAPCOM** **(CONTINUES WITH PASSION).** Kwa hivyo kuanzia leo na kwa muda wa juma moja lijalo, tutakuwa tukiwapa muda wa dakika 10 tu kufungua tovuti mbalimbali bila malipo

**81. GEORGE** **(LOUD WHISPER IN PANIC)** Kwani una wazimu?

**82. ZAPCOM** Dakika 10, sisi zote hapa, kufungua tovuti za burudani na elimu.

**83. ALL** **GROANS**

**84. ZAPCOM** Lakini hamtagharamia muda huo? Ni bure. Hebu tuanze.... Andika www.dw-world.de/lbe .

**85. K-SFX: RAPID TAPPING OF KEYBOARD AND MURMURING**

**86. ZAPCOM** **(AUTHORITAVELY)** Haiwezekani,kwa muda huo kufungua, kusoma na kusikiza vipindi vya redio vya "Learning By Ear" . Hebu fikiria jambo linaloweza kuwasaidia. Bado nina kazi ya kufanya!.

87. **UNCLE KILU** **(SUPRISING THEM-CLEARS THROAT)....** Kundi hili la vijana linakutegemea wewe kwa ushauri na muongozo. Chukua (**CLATTER**)... hii hapa supu ya mbuzi!.

**88. ANNOUNCER** Ama kwa hakika , huduma za mtandao wa Intaneti ni za manufaa makubwa kwa habari za kuelimisha na burudani, lakini, pia kuna habari na picha nyingine zinazopatikana humo ambazo ni za aibu. Ungana nasi wakati mwengine kwa kipindi kijacho ili ufahamu mengi yatakayojiri. Pia unaweza kutembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe Hadi wakati huo kwaheri kwa sasa.